



SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 1
SWAHILI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1
SWAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1

Thursday 3 November 2005 (morning)

Jeudi 3 novembre 2005 (matin)

Jueves 3 de noviembre de 2005 (mañana)

1 h 30 m

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

KIFUNGU A

MASHABIKI WAJITOKEZA KUSHUHUDIA UZINDUZI WA VIDEO YA TOUCHBOY

Na Kazungu Samwel

Mamia ya wakazi wa Mombasa na ambao ni mashabiki sugu wa muziki wa kizazi kipywa, walijazana Sea-Horse Hotel, Bombolulu, Mombasa, kushuhudia "live" uzinduzi wa kanda ya video ya vijana wawili machachari wa Mombasa Touchboy na Mad-Mosh.

Kulingana na meneja, Bw.Willy Kenani, watu zaidi ya 400 walishuhudia uzinduzi wa kanda hiyo ya video, *Anazungusha*, mwishoni mwa wiki. Bw. Willy alisema kuwa mtiririko wa mashabiki uliofika kushuhudia hafla hiyo ni dalili wazi kuwa vijana hawa wametokea kuwa kivutio cha wengi.


'Ni wazi kuwa vijana hawa sasa wamejenga milki kubwa ya mashabiki na ikiwa mambo yataendelea kuwa hivi, basi huenda vijana hawa wakapiga hatua kubwa siku za usoni,' alisema.

Ingawa uzinduzi wenyewe ulianza saa tano usiku, mashabiki walianza kumiminika ndani ya ukumbi tangu saa moja jioni. Ilipofika saa tatu, tayari ukumbi ulianza kulemewa na mashabiki. 'Daima hapa huwa na shoo tofauti tofauti lakini hii ya leo imekuwa kali zaidi,' alidai shabiki ukumbini.

Kabla ya Mad-Mosh na Touchboy kuingia jukwaani, wasanii ambao walikuwa wamealikwa kutumbuiza walisisimua vilivyo kadri walivyojimwayamwaya ukumbini. Miiongoni mwa wasanii waalikwa alikuwa mwanarapa machachari Tazzboy, ambaye kwa kweli aliwaacha mashabiki hoi kwa miondoko yake ya *Dance hall*. Wengine waliohuduria walikuwa ni kikundi cha rap cha City Crook na mwanadada maarufu wa chakacha mjini Mombasa, Lady Super.

Ilikuwa ni furaha zaidi wakati mwanadada Lady Super alipojitoma ukumbini na kuanza kunengua kiuno chake katika miondoko ya chakacha. Ni dhahiri aliwatia kiwewe mashabiki ambao walianza kuacha viti vyao huku wengine wakijaribu kwenda jukwaani kumgusa ingawa hilo halikutimia kutokana na ulinzi maridhawa. Kila alipogeuka kwa staili tofauti za minengu yake, wengi walipiga mbinja, huku wakishangilia. Huyu Lady Super anatutia wazimu! Hebu ona vile anavyofanya pale jukwaani, alidakia mtu mmoja.

Mad-Mosh na Touchboy walijibwaga jukwaani saa tano usiku na kuanzisha rasmi kanda yao kwa mbwembwe za kipekee. Walitumia fursa hiyo kutoa rasmi wimbo wao wa pili, *Cheki dada*, ambao ni mchanganyiko wa *hip-hop, raga* na *Dance hall*.



KIFUNGU B

NGUVU YA MAPENZI

‘Lo! Nawe shemeji umenitia wasiwasi kweli. Niliondoka kabla hujarejea tangu uende kununua gazeti. Nikamwachia bawabu ufunguo wa nyumba. Niliporejea toka kazini ananieleza hajakuona tangu asubuhi.’

‘Gazeti sikupata’, nikajibu. ‘Kila nilipoenda nilikuta polisi wamesomba magazeti. Kisha nikapotea njia. Nilidhani mambo ni ya mkono kumbe ni upembo.’

Tim aliniangalia kwa mshangao hata zaidi.

‘Ooh! Maskini! Pole Akida’, alisema huku kakazia macho miguu yangu mitupu.

‘Alaah! Na viatu umeviacha nje?’

‘Vimeibwa’, nikajibu kwa hofu na hisia za hatia.

10 ‘Umepata ubatizo wa jiji’, alisema Tim kwa stihizai.

Tim akaangua kicheko kikubwa. Tim alicheka mpaka akaanguka kitandani na kuendelea kucheka. Nilikuwa nategemea kukaripiwa na kuzomewa kwa ushamba wangu uliopelekea kupotea kwa viatu vya rafiki yangu Tim. Badala yake Tim alikuchukulia kupotea kwa platifomu zake kama jambo ndogo. Nilishangazwa mno na moyo wake mweupe na mwingu wa msamaha.

15 ‘Usijali Akida’, alisema.

Kisha tulisikia mlango wabishwa. Tim akaamka kwenda kuufungua.

‘Ai! Pam!’ Tim alipaza sauti alipoufungua mlango wa kijumba chake na kumwona mchumba wake amesimama mlangoni.

‘Kwa nini washangaa?’ Pamela alimwuliza, huku akitabasamu.

20 ‘Paam... ume... umefika?’ Tim aligugumia, moyo haukuwa wake. ‘Karibu’.

Pamela aliangua kicheko kikubwa. Langu jicho tu.

Mtu kwa kumwona tu mpenzi wake kapata kigugumizi! Nyumba iliyokuwa safi ndani tangu hapo, ilikuwa safi zaidi, kila kitu mahali pake. Wawili wapendanao walikumbatiana na kudoneana kimyakimya. Pam, kama alivyoitwa na Tim, alikuwa mwembamba wa umbo, mweusi pi na mwenye macho yenye haiba ya lulu za pwani. Wasichana wapatikanao kwenye majalada ya Waremo, hawaambui chochote wakilinganishwa na Pam. Kaumbwa kaumbika. Nadhani hili ndilo lililomkosesha Tim kauli.

Jioni hiyo tulikula vyakula vilivyopikwa vikapikika. Pam alikuwa mpishi hasa; sijui kasomea Sayansi Kimu shulenii. Tuliporoja na kuangua vicheko sio kidogo. Pam na Tim walizungumza mengi juu ya ndoa yao, mustakabali wao, matamanio yao na itikadi zao. Kigugumizi cha Tim cha muda kilipotea taratibu akawa amestarehe na kuupata ufasaha wake.

30 ‘Wakati wa uchumba ni wakati hatari sana’, alitongoa Tim.

‘Wakati wa uchumba ndio wa kutathmini mtu umpedaye’, alisema Pam.

‘Ni wakati wa kupanga mikakati ya maisha yenu ya halafu. Eee! Kuoneshana mahaba. Ni wakati wa kuwasha mshumaa wa mapenzi yasiyojua kuzimwa yakazimika.’

35 ‘Umekosea Pam’, alidakia Tim baina ya kicheko tulichokuwa twacheka sote. ‘Uchumba pia ni wakati wa kufumbia macho makosa ya mchumba. Wakati wa Kufikiri mtu ni maasumu. Hukumbuki Kasisi John anavyotutahdarisha kwenye mahubiri yake mara nyngi? Alisema pia Wakristo wanaochumbiana wanaweza kupoteza udhibiti wa utashi wao... Wakajikuta wamefanya dhambi kama vile Daudi na mke wa Uriia.’

40 Kimya kikajiri kitambo. Niliutazama uso wa Pam, nikaona umepiga matuta na macho kamtumbulia mchumba wake.

Ken Walibora, *Kufa Kuzikana*, 2003

KIFUNGU C**UGONJWA WA MTOTO WA MFALME**

Ugonjwa wa mtoto wa Mfalme uliendelea. Uso wake mzuri wa takaso ulifisia. Macho yaliingia ndani kwa kukonda, mifupa ya taya ilitokeza nje, mashavu yalibonyea, mabega yalichongoka, na mwili ambao ulikuwa wa umbo la mviringo sasa ulibaki mifupa iliyojionyesha katika ngozi.

- 5 Mganga baada ya mganga alikuja na kwenda zake. Dawa baada ya dawa ilitumiwa lakini nafuu ilichelewa kutokea. Wakati huu wote Mfalme wa Kufikirika hakusahau kuwa katika utabiri wa uzazi wa mwanawewe, alikuwa amelazimishwa na hamu ya kuzaa kuweka nadhiri ya kumwaga damu ya watu wawili kwa kafara. Jambo hili lilikuwa limetokea miaka kumi na moja iliyopita. Ililazimu sasa yeze kutimiza upande wake wa ahadi ya nadhiri ambayo
10 10 alisadiki kuwa imemtimizia hamu yake maridhawa. Kutekeleza ahadi ni jambo la lazima kwa kila mtu kwani neno la mtu ndiyo pingu yake.

Kwa mtu mtukufu kama alivyokuwa yeye, wajibu wa kutimiza ahadi ni mkubwa mno. Lakini alikumbuka vilevile kuwa sheria za nchi yake zilikuwa haziidhinishi kumwaga damu ya mtu hata mmoja, licha ya watu wawili, kwa kafara. Mwanawewe alikuwa ana haki ya mapenzi
15 15 yake ya kwanza. Pia ni wajibu wa kila mtu bora kwanza kuwapenda jamaa zake. Raia walitegemea himaya yake, na sheria za nchi zilitaka utii wake vilevile. Mambo haya yote yalikuwa katika mikono yake. Cha shina kitamu, cha kati kitamu, na cha ncha kitamu.

Hapa, nadhiri ilidai kafara la damu ya mtu. Sheria za nchi zilipinga kafara hii. Mfalme alitatizwa sana wakati alipokuwa akifikiria njia za kutimiza ahadi yake kubwa. Ilikuwa ni
20 20 ahadi kubwa kweli kwa sababu mbele yake kulisimama pingamizi.

Waziri mkuu aliita kikao cha dharura cha Baraza la mawaziri, makadhi, mastadi wa kujadiliana, wanachuoni, mahatibu na wakulima mashuhuri.

Alisema, ‘Mtoto wa mfalme wetu ni mgonjwa kitandani. Mikoba ya waganga wetu wote bora imemimina dawa zote zilizokuwemo ndani yake. Haikutokea hata dawa moja kuwa
25 25 mujarabu. Hatari ya maisha ya mtoto inahofiwa sana. Mfalme anastahili msaada wa kila raia. Wanatakiwa watu wawili, mwerevu na mjinga, kwa kafara.’

Viongozi wa dini walisema kuwa hawakuweza kuona njia ya kuidhinisha kafara ya damu ya mtu. Wanasheria walionyesha kuwa kafara ya damu ya mwanadamu ikiidhinishwa katika sheria itatia
30 30 watu wote katika mauaji. Wanachuoni walisema kuwa nchi nydingi zimechafuka kwa mauaji. Wakulima walieleza kuwa kuua mmea ni kukaribisha njaa katika nchi. Kadhalika, kuua mtu kwa kafara kutaleta maasi katika nchi. Mfalme alijikuta kwenye njia panda.



KIFUNGU D

USALAMA KATIKA MITAA YA MABANDA

Na Maitha Masha

Usalama katika mitaa ya mabanda ni mfano wa kitendawili kisichokuwa na jibu. Utatoka wapi ilhali huko ndiko wanakoishi wahalifu wa kila aina? Ni katika sehemu kama hizo ambapo ni marufuku kwa mtu yeyote kununua radio na televisheni. Wezi huvamia punde tu wanapojuia katika nyumba fulani kumenunuliwa kimoja cha vifaa hivyo.

Katika baadhi ya mita hiyo ya mabanda, wezi hutumia bunduki kupora wenyewe vyakula, kama vile unga na mafuta ili wakavitumie nyumbani kwao. Asilimia kubwa ya visa vya mauaji na ubakaji vinavyoripotiwa jijini Nairobi hutekelezwa katika mitaa ya mabanda.

Je, ni kwa nini maovu yote ya jamii yanapatikana katika mitaa hiyo? Jibu ni Umaskini. Wengi wanaoishi katika mitaa hii ni watu wasiokuwa na kazi. Walio na bahati hupata kazi za kibarua katika eneo la viwanda ambako wanapata malipo duni yasiyotosheleza mahitaji yao.

Je, watu hawa wasiokuwa na kazi hula nini? Kutokuwa na kazi ni mionganini mwa hali zinazochangia visa vya wizi. Mtu asiyekuwa na kazi akihisi njaa inambidi aibe. Asilimia kubwa ya wizi katika sehemu kama hizo hutekelezwa na watu walio na njaa amba wanatafuta chakula tu.

Lakini uhalifu katika mitaa ya mabanda ya Nairobi hautekelezwi kwa sababu ya njaa pekee. Ripoti kutokana na uchunguzi wa mashirika mbalimbali nchini unaonyesha kuwa dawa za kulevyaa zinachangia uhalifu katika jamii. Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari, idadi kubwa ya dawa za kulevyaa hufichwa katika mitaa ya mabanda kwa sababu sio rahisi kupatikana na polisi.

Mbali na dawa za kulevyaa, Pombe haramu, ikiwemo chang'aa, huuzwa kwa wingi katika mitaa ya mabanda. Kwa sababu wakazi wengi hawana kazi, njia ya pekee ya kutumia wakati wao ni kunywa pombe hiyo na kutumia dawa.

Mlevi ni mlevi tu na anaweza kufanya lolote kwa sababu ya ulevi. Visa vingi vya mauaji, ubakaji, wizi na ugomvi wa nyumbani katika mitaa ya mabanda hutekelezwa na walevi wa pombe au dawa. Hali hiyo ilikuwa mbaya zaidi kabla ya 2003 kwa sababu vijana wengi hawakuwa wakienda shuleni kwa kukosa karo. Lakini sasa wengi wao wamejiunga na shule tangu serikali ilipoanzisha elimu ya bure katika shule za msingi.

